

Upimaji wa UVIKO-19 hapa Nova Scotia

Upimaji unapatikana kwa Wanova Scotia wote wenye dalili. Wanova Scotia wengi wanaweza kupata kipimo cha haraka cha antijeni, wakati wale walio katika hatari kubwa ya kuugua vibaya na wafanyakazi wa kazi fulani pia wanaweza kupata kipimo cha PCR (maabara).



Klipimo cha PCR

Kinapatikana kwa watu ambao wana dalili NA wako katika hatari ya kuugua vibaya. Weka miadi ukitumia zana ya kujitathmini mtandaoni au piga simu 811. Angalia kama unastahiki PCR kwenye nshealth.ca/coronavirustesting.

Unaweza kufikia matokeo yako ya kipimo cha PCR (hasi, chanya na isiyojulikana) ikiwa una kadi halali ya afya ya mkoa (kutoka mkoa wowote), kitambulisho cha mwanafunzi au nambari nyingine ya usajili, kwa njia zifuatazo:

Barua pepe	Matokeo ya barua pepe yanaweza kupokelewa saa 24 kwa siku. Angalia faili lako la "Junk" kwa matokeo yako ya kipimo. Tegemea barua pepe kutoka noreply@nshealth.ca. Ni muhimu kujitathmini na anwani sahihi ya barua pepe (iangalie mara mbili unapofika kwenye kipimo chako. Haiwezi kubadilishwa mara tu unapopimwa.
Simu ya kiotomatiki	Ikiwa hutafikia matokeo yako kwa barua pepe, utapokea simu ya kiotomatiki – mara nyingi kati ya saa 8 mchana na saa 11 mchana. Ikiwa unasubiri matokeo ya kipimo, weka simu karibu nawe na iwashie. "kitambulisho cha mpigaji" kinaweza kuonyesha kama nambari isiyojulikana, jina lisilojulikana la nje ya mkoa. Tafadhali jibu. Simu ya kiotomatiki itajaribu mara mbili.
Mtandaoni	Ili kufikia matokeo yako mtandaoni tembelea c19results.nshealth.ca
Simu	Utapokea simu kutoka Afya ya Umma na matokeo yako ikiwa huna kadi halali ya afya ya mkoa au hatuwezi kukufikia kupitia njia zingine zilizoordheshwa hapo juu.



Ikiwa ni Hasi

- Kaa nyumbani ikiwa bado una dalili.
- Fuata maagizo kwenye nshealth.ca/i-have-covid-19-symptoms



Ikiwa ni Chanya

- Fuata maagizo kwenye nshealth.ca/testedpositiveforcovid
- Jaza Ripoti na fomu saidizi za uchunguzi kwenye c19hc.nshealth.ca/self-report au piga **1-833-797-7772** ikiwa huna mtandao au unahitaji usaidizi.



Ikiwa haijulikani

- Ikiwa una dalili unahitaji kuomba miadi ya kipimo kingine kwenye covid-self-assessment.novascotia.ca/en



Ili kufikia matokeo ya kipimo unahitaji kuingiza tarakimu nne za mwisho za kadi yako ya afya au kitambulisho. Matokeo ya kipimo kwa kawaida hupatikana ndani ya siku 1-3. Iwapo imekuwa zaidi ya saa 72 piga simu Afya ya Umma 1-844-996-0694.

Matokeo ya kipimo yasiyojulikana yanamaanisha kuwa kipimo chako cha mwisho hakikuonyesha matokeo dhahiri kama chanya **AU** hasi.

Hakikuweza kutambua UVIKO-19 kwa usahihi. Matokeo yako yanaweza kuwa yasiyojulikana ikiwa:

- Kwa sasa umeambukizwa UVIKO-19 lakini kipimo kilifanyika mapema sana kugundua virusi
- **AU** uliambukizwa UVIKO-19 hivi karibuni na kipimo kinagundua kiasi kidogo cha virusi visivyoweza kuepukika (vilivyokufa)
- **AU** kulikuwa na tatizo na sampuli yako au kipimo chenyewe.

Upimaji wa haraka wa Antijeni

Unapatikana kwa watu ambao wana dalili lakini hawako katika hatari kubwa ya ugonjwa mbaya.

Weka miadi kwa kutumia zana ya kujitathmini mtandaoni ili kuchukua vipimo vya haraka kwenye kituo cha kupimia.

Chukua kipimo cha haraka bila miadi katika ofisi za MLA na maktaba. Kinapatikana pia Access NS na Feed Nova Scotia kwa watu wanaotumia huduma zao.

Maagizo ya jinsi ya kutumia vipimo vya haraka yanapatikana kwenye nshealth.ca/coronavirus/covid-19-rapid-testing

Vipimo vya haraka vinapaswa kutumika tu ikiwa una dalili. Vipimo viwili hasi vya haraka vilivyochukuliwa masaa 48 kati yavyo inachukuliwa kuwa hasi (hakuna maambukizi)

Ikiwa utapata matokeo chanya, tembelea c19hc.nshealth.ca/self-report na ujaze Ripoti na fomu saidizi ya uchunguzi ili kusaidia kutambua kwa haraka watu wanaostahiki na wanaweza kufaidika na dawa za UVIKO-19. Kisha tembelea nshealth.ca/testedpositiveforcovid kwa taarifa kuhusu jinsi ya kupunguza kuenea kwa virusi.

Iwapo unahitaji kupimwa UVIKO-19 kwa ajili ya Kusafiri au kwa madhumuni ya kazi utahitaji kutembelea kliniki ya kibinafsi ya upimaji (nshealth.ca/coronavirus-home/i-need-covid-test-travel).

Kwa taarifa tembelea: nshealth.ca/coronavirustesting

Updated June 24, 2022

